






Salamu + Hisia + Maumbo Greetings, Feelings and Shapes




Duara



Duaradufu



Pembetatu



Msambamba



Mraba




Nusuduara




Tenge




Mstatili




Pembetano



Pembesita



Msalaba




Pembenane



Moyo



**Hilali
(Mwezi)**




Pete



Nyota



Mstari



Mshale

UTANGULIZI

Introduction

Wewe ni nani?

Una miaka mingapi?

Unaishi wapi?

Unasoma shule gani?

Wewe unatokea wapi?

Unapenda nini?

Who are you?

How old are you?

Where do you live?

What is the name of your school?

Where are you from?

What do you like?

KUHUSU MIMI

About me...

Jina langu ni.....

My name is...

Mimi nina miaka.....

I amyears old

Mimi ninaishi.....

I live at...

Jina la shule yangu ni.....

The name of my school is

Mimi ninatokea.....

I am from....

Mimi Ninapenda.....

I like/ love to....

SOMA NA CHORA MAUMBO KAMA SOFIA!

Alfajiri na Mapema - Amka, Amka!
Early in the morning -Wake up! Wake up!

Sofia: Shikamoo Baba

Sofia: Hello Dad

Baba: Marahaba mwanangu. Umeamkaje?

Dad: Hello my child. How did you wake up?

Sofia: Salama baba. Na wewe je?

Sofia: I am well, and you?

Baba: Mimi sijambo pia. Unajisikiaje leo?


Dad: I am well too. How are you feeling?

Sofia: Nina furaha sana.

Sofia: I am so happy.

READ AND DRAW THE SHAPES LIKE SOFIA!

Sofia ana furaha. Yeye anachora saa ya duara
Sofia is drawing a round watch.



Asubuhi: Saa ya chai
Morning: Breakfast time


Dada: Habari za asubuhi Sofia?
Sister: How is your morning Sofia?

Sofia: Nzuri, za kwako?
Sofia: Good. how about you?

Dada. Safi tu. Karibu mezani
Sister: Good likewise, welcome to the table.

Sofia: Asante dada. Nakuja
Sofia: Thank you sister, I am coming.

Sofia ana njaa. Yeye anachora biskuti ya mraba
Sofia is hungry. She is drawing a square cookie.



Baadaye: Saa ya shule
Afterwards: School time

Kaka: Mambo vipi Sofia?
Brother: How are you Sofia!

Sofia: Poa kaka. Na wewe je?
Sofia: Good. How about you?


Kaka: Poa. Unaenda shule leo?
Brother: Are you going to school today?

Sofia: Ndio. Ila naogopa. Ni siku ya kwanza leo.
Sofia: Yes. but I am scared. It is my first day today.

Kaka: Usiwe na wasiwasi mpendwa. Twende pamoja
Brother: Don't worry my dear. Let's go together.

Sofia: Sawa kaka. Twende zetu.
Sofia: Sure brother, let's go

Sofia ana woga. Yeye anachora alama ya shule ya pembetano
Sofia is scared. She is drawing a pentagon school sign.



Saa ya Mapumziko:
Break/ Recess Time

Sofia: Shikamoo Mwalimu

Sofia: Hello Teacher

Mwalimu: Marhaba Sofia. Habari za leo?

Hello Sofia, how are you today?

Sofia: Nzuri, lakini nimechoka.

Good, but I am tired.

**Mwalimu: Pole sana. Ni saa ya mapumziko
sasa.**

Teacher: Sorry about that. It is break time now.

Sofia: Ahaaa! Mimi naenda kucheza nje.

Sofia: Aha! I am going to play outside.

Mwalimu: Sawa. tutaonana baadaye


Teacher: Perfect, see you later.

Sofia: Sawa. Kwaheri Mwalimu

Sofia: Cool, bye teacher.

**Sofia amechoka. Yeye anachora kipande cha jibini cha
pembetatu**

Sofia is tired. She is drawing a triangle cheese piece



Mchana:Saa ya kula
Afternoon: Lunch time

Sofia ana njaa. Yeye anachora yai la duaradufu
Sofia is hungry, she is drawing an oval egg

Sofia: Habari za mchana Zara?

Sofia: Good afternoon Zara!

Mwanafunzi (Zara): Nzuri. Za kwako?

Student (Zara): Good. How about you?

Sofia: Safi tu! joto sana leo.

Good. too hot today!

Zara: Ndio. halafu nina njaa!

Zara: True. and I am so hungry!

Sofia: Mimi pia. Leo ninakula mayai.

Sofia: Me too. Today I am eating eggs.

Zara: Oh! Vizuri. Mimi ninakula wali kuku

Zara: Oh!Great. I am eating rice and chicken

Sofia: Mlo mwema eh!

Sofia: Enjoy your meal eh!

Zara: Mlo mwema pia.

Zara. Enjoy your meal too.

Saa Saba Mchana Saa ya kupumzika:
One O'clock(PM): Nap Time

Sofia amechoka. Yeye anachora kitanda cha mstatili
Sofia is tired. She is drawing a rectangle bed.

Emma: Vipi Sofia?

Emma: what's up Sofia?

Sofia: Hamna mpya Mambo vipi?

Sofia: Nothing new, how are you?

Emma: Powa. unajisikiaje?

Emma: cool. How are you feeling?

Sofia:Nimechoka. Nasinzia nimekaa.

Sofia: I am tired. I am sleepy while sitting.

Emma: Pumzika kidogo rafiki yangu

Emma: Take a little rest my friend

Sofia: Sawa. Naenda kulala kidogo


Sure. I am going for a nap.

Emma: Powa, usingizi mwema.

Emma: Cool, good nap.

Sofia: Asante. Kwaheri Emma.

Sofia: Thanks. Bye Emma.



Alasiri Saa ya kuamka
Late afternoon: Wake up time

Sofia ana homa. Yeye anachora nyota.
Sofia has fever. She is drawing a star

Mwalimu (kwenye simu): Haloo mama Sofia
Teacher(On the phone): Hello Sofia's Mom

Mama Sofia: Hallo, mwalimu. Habari za leo?
Sofia's Mom: Hi Teacher, how are you today?

Mwalimu: Nzuri. Ila kuna tatizo kidogo.
Teacher: Good. But there is a small problem.

Mama Sofia: Nini tena jamani?
Sofia's mom: What is the wrong?

Mwalimu: Sofia ana homa kali. Nampeleka hospitali ya shule
Teacher: Sofia has a high fever. I am taking her to the school hospital.

Mama Sofia: Asante kwa kunijulisha, nakuja sasa hivi hapo hospitali.
Sofia's mom: Thanks for letting me know, I will soon be coming at the hospital.

Mwalimu: Sawa. Tutaonana baadaye
Teacher: Okay, see you later.

Saa tisa na nusu: Saa ya kwenda hospitali
Three thirty PM: time to go to the hospital

Sofia ana wasiwasi .Yeye anachora moyo.
Sofia is worried. She is drawing a heart

Mwalimu: Sofia, unajisikiaje?

Teacher: How are you feeling Sofia?

Sofia: Naumwa kichwa

Sofia: I have a headache

Mwalimu: Pole sana Sofia

Teacher: I am deeply sorry Sofia.

Sofia: Asante mwalimu

Sofia: Thank you Teacher

Mwalimu: Twende hospitali.

Teacher: Lets go to the hospital

Sofia: Jamani! Mimi naogopa sindano

Sofia: Oh my! I am afraid of needles

Mwalimu: Hapana. Usiogope. Mama yako anakuja pale pia

Teacher: No, don't be scared. Your mom will be coming too.

Sofia: Afadhali. Sawa, twende.

Sofia: That's better. Ok, let' go.

Baadae Jioni: Saa ya kusoma.
Later in the evening: Reading time

Sofia ana kiu. Yeye anachora boksi la jusi la mraba
She is drawing a square juice box

Rafiki (Rosa): Mambo Sofia?
Friend (Rosa) Hi Sofi?

Sofia: Poa rafiki yangu! Za kwako?
Sofia: Hi my friend! How are you?

Rosa: Poa. Unajisikiaje?
Rosa: Cool. How are you feeling?

Sofia: Nina kiu. Naomba maji tafadhali
I am thirsty. May I have some water please?

Rosa: Usijali. Mimi nina chupa mbili leo.
Unaweza kuchukua moja.
Rosa: Dont worry, I have two bottles today. You can take one.

Sofia: Asante sana rafiki! Nakupenda.
Sofia: Thanks a lot my friend. I love you

Rosa: Nakupenda pia
Rosa: I love you too

Usiku Saa ya kwenda nyumbani.
At Night: Time to go home

Daktari: Mama Sofia, mwanao anaendelea vizuri sana. Mnaweza kwenda nyumbani.

Doctor: Your child is doing much better, you can go home.

Mama Sofia: Asante daktari. Asante sana.

Mama Sofia: Thank you doctor, nashukuru sana.

Mama Sofia: Sofia, Sofia mwanangu, unajisikiaje sasa?

Mama Sofia: Sofia, my daughter, how are you feeling now?

Sofia: Najisikia nafuu

Sofia: I feel better

Mama Sofia: Nafurahi kusikia hivyo. Tumeruhusiwa, tunaenda nyumbani.

Mama Sofia: Glad to hear that. We have been discharged; we are going home.

Sofia: Sawa mama. Nafurahi homa imeisha.

Sofia: Ok mom. I am happy the fever is gone.

Sofia anatabasamu. Yeye anachora mshale.
Sofia is smiling. She is drawing an arrow

